nystateofhealth™
The Official Health Plan Marketplace



# UNASTAHILI HUDUMA YA AFYA UNAYOWEZA KUMUDU

NY State of Health ipo hapa kukupa msaada wa binafsi wa kupata mpango sahihi na msaada wa kifedha ili kupunguza gharama zako.

## KATIKA NY STATE OF HEALTH 'UTAPATA

1. Mipango mingi ya afya bora unayoweza kumudu
2. Msaada wa binafsi wa kuchukua mpango wako
3. Msaada wa kulipia mpango unaochagua
4. Essential Plan (Mpango Muhimu) kwa watu wa mapato ya chini

## KUJISAJILI NI RAHISI! KUWA NA HABARI HII YA KILA MWANAFAMILIA YAKO

- Tarehe za kuzaliwa
- Namba za usalama wa jamii au, kwa wahamiaji wa kisheria, namba za nyaraka iwapo zipo
- Uajiri, rekodi za mapato, na Habari ya bima ya afya

**JISAJILI SASA!**
1-855-355-5777 au
TTY: 1-800-662-1220

nystateofhealth.ny.gov
Msaada wa bila malipo wa kibinafsi

nystateofhealth™
The Official Health Plan Marketplace

# THE ESSENTIAL PLAN (MPANGO MUHIMU)

Essential Plan (Mpango Muhimu) ipo kwa ajili ya watu wa New York walio na mapato ya chini.

Kwa wengine, inagharimu kiasi cha chini ya dola kwa siku. Kwa wengine, haigharimu chochote.

NA HAUNA MAKATO, kwa hivyo mpango unaanza kulipia huduma ya afya yako mara moja.

## ESSENTIAL PLAN (MPANGO MUHIMU) HUTOA FAIDA ZIZO HIZO BORA KAMA TU MIPANGO MINGINE

- Ziara za daktari, ukijumuisha wataalamu
- Vipimo vilivyoagizwa na daktari wako
- Maelekezo ya dawa
- Huduma ya kulazwa na ya kutibiwa na kuondoka hospitalini

**Chini ya Essential Plan (Mpango Muhimu), sehemu unayolipia kila huduma ya afya – mlipiaji mwenzako – ni ya chini sana. Na wakati mwingine, hata ni $0.**

**Na hulipii chochote kwa ajili ya huduma za uzuiaji, kama vile vipimo vya daktari vya kawaida na uchunguzi.**

Jisajili kwa Essential Plan leo. Usajili upo wazi **MWAKA MZIMA.**

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Serikali kuu na za jimbo zinazotumika na haibagui kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya taifa, imani/dini, jinsia, umri, hadhi ya ndoa/familia, kufungwa kwa uhalifu,, utambulisho wa jinsia, mvuto wa jinsia, tabia za kijeni, hali ya jeshi, dhuluma za nyumbani na/au kisasi.

11163 (Swahili) 10/18